SOMO LA 9

MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU MBINGU NA KUZIMU (HELL)

“Maana watenda mabaya wataharibiwa, Bali wamngojao BWANA ndio watakaorithi nchi… Wenye upole watairithi nchi” (Zaburi 37:9-11).

“HELL” – “KUZIMU” katika Biblia si zaidi ya kaburi. Mbingu ni kiti cha enzi cha Mungu.” Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni.” NCHI ndiyo imehaidiwa mtu kama zawadi yake: “Wapole watairithi NCHI.” Vifungu ambavyo vimenukuliwa katika somo la 8 vimeonyesha bila kutilia shaka kuwa wafu wamekufa hakika, na katika hali hiyo hawajashuhudia {malipo} wala adhabu, maana hawana uhai wa namna yoyote. Wanajilalia katika makaburi yao, wakisubiri ufufuo.

Pia hakuna ahadi yoyote katika maandiko kwa mtu yeyote kupata nafasi ya kwenda mbinguni wakati wowote. Ahadi ya Biblia yazungumzia tu kufanywa upya kwa nchi; kujazwa kwa utukufu wa Mungu. Ni kweli Petro anena juu ya –

“Urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu” (1 Pet. 1:4)

Mtu anaweza kurukia wazo la kupata malipo mbinguni. Yesu vilevile alisema.

“Thawabu yenu ni kubwa mbinguni… Jiwekeeni hazina mbinguni” (Mathayo 5:12;6:20)

Kusema kweli thawabukwa sasa “imehifadhiwa mbinguni,” ikisubiri kutolewa wakati fulani siku za usoni. Kitu kinapohifadhiwa, huwekwa mahali salama, mahali teule hadi itakapotakiwa, na huletwa: kama vile Benki kuu inavyohifadhi fedha na kuzitoa kwa benki ndogo ndogo zinapohitajika. Hivi basi Petro anaendelea kusema vifungu vichache baadaye kuhusu ile zawadi iliyohifadhiwa:

“Ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo” (vifungu 13)

Na Yesu anayakariri haya –

“Naja upesi, na ujira wangu U PAMOJA NAMI (Ufunuo 22:12).

“Utalipwa katika ufufuo wa wenye haki” (Luka 14:14).

Na Paulo anatupa taswira au picha mfano huu Kristo atakapokuja –

“Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake… taji na haki, atanipa siku ile… na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake”(2 Timotheo 4:1,8)

Ni wazi kuwa thawabu hii haiji kabla ya hukumu. Biblia yaeleza kivingine, kama ambavyo maandiko yaliyonukuliwa yanavyoonyesha kufikiria hapa.

Ukweli wa mambo ni kuwa Kristo yuaja na ujira, na kuwa kwa sasa yuko mbinguni, ni wazi basin a ni sawa kusema zawadi imehifadhiwa mbinguni. Kipengele kimojawapo cha zawadi ni utawala pamoja na Kristo atakaporudi, kama tutakavyoona. Hakuna mtu ambaye amezawadiwa hivyo kuwa sasa ni jamboo bayana.

Fikiria juu ya eneo la hukumu katika Mathayo 25:31-46 –

“Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake”

- Halafu anawakaribisha wenyehaki katika ufalme wake. Fikiria pia aliyosema katika Yohana 5:28-29, kuwa waliokufa watatoka katika makaburi yao ili wazawadiwe uzima au mauti. Haya yatawezekana vipi ikiwa tayari wamepata zawadi zao mbinguni au kuzimu, miaka mingi kabla ya majilio ya Kristo?

Hakuna uzao wa Adamu (isipokuwa Kristo mwenyewe) amewahi kupata nafasi, au ahadi, ya kufikia makao ya Mungu katika “mbingu za mbingu.” Yesu alimwambia Nikodemu –

“Wala HAKUNA MTU aliyepaa mbinguni” (Yohana 3:13)

Juu ya Daudi mwaminifu, mwandishi wa zaburi (ametajwa kama mtu ambaye roho wa Mungu yaambatana naye), imeonyeshwa wazi kuwa hata yeye hakwenda mbinguni. Hakika kama palikuwa na nafasi ya kupata heshima hiyo ya kwenda mbinguni, Daudi hakustahili kuikosa. Biblia yasemaje?

“Baba yetu mkuu Daudi… alifariki, akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo … Maana Daudi hakupanda mbinguni (Matendo 2:29 - 34)

Kifungu hiki kinaashiria ukweli kuwa Kristo alipaa mbinguni kama thibitisho yeye ni masihi.

Kuongeza kwa orodha ndefu ya watu waaminifu,wenye imani katika Waebrania II, Ikijumuisha Ibrahim, Isaka, Yakobo, Daudi, n.k –

“Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi: kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi” (Waebrania 11: 39-40).

Hapa kuna maelezo wazi kuwa Daudi na waaminifu wengine hawajapokea ahadi zile, wala hawajakamilika na itakuwa hivyo hadi waaminifu wajao wapate pamoja nao (wakati wa ufufuo Siku ya Mwisho).

Tuna watu wawili wanaotajwa na habari ya vifo vyao ni tatanishi. Kuhusu Henokotunaelezwa:”Henoko alihamishwa asiye akaona mauti,” (Waebrania 11:5). Na juu ya

Eliya: Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli" (2 Wafalme 2:11). "Mbingu" inatumiwa kwa namna mbalimbali ("ndege na mbinguni au angani," "Mvua kutoka mbinguni"), na hii "mbingu" aliyopaa Eliya ni bayana si "mbingu ya mbingu" kiti cha enzi cha Mungu, kwani hakuna aliyepaa huko, kama tulivyokwisha kuona. Mahali walipo hawa wawili hatupajui. Hatuajaambiwa. Mambo yao ni ya kipekee: kulingana na maandiko ni kama hawakufa. Alichowaandalia Mungu, hajatufunulia. Lakini hawa wawili mambo yao ni ya kipekee, sio kawaida. Kwa kuwa suala lao ni tofauti, haliambatani na sisi wengine tunaokufa.

Yesu alipokuwa akimliwaza Marita juu ya Lazaro (aliyekuwa amekufa), hakumwambia, kama wengine wafanyavyo siku hizi, kuwa ana furahia utukufu wa mbinguni; bali alimpa moyo kwa kumwambia, kwa mtindo wa kweli wa maandiko: "Ndugu yako atafufuka" (Yohana 11:23)

Paulo pia aliyatumia maneno ya namna hii ya kuwaliwaza makiwa kuhusu mafundisho ya ufufuo. Hakufunza kuwa wafu wameenda kwenye raha ya milele au adhabu ya moto. Kwa waombolezaji Wathesalonike, alisema (1 Wathesalonike 4:13 - 18) –

"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti… Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni… nao waliokufa katika katika Kristo watafufuliwa… Basi farijianeni kwa maneno hayo."

Ingelikuwa vigumu sana kuyatamka haya kama wangelikuwa hai katika raha mbinguni.

Kusudi kwa Kristo mara ya pili, na ufufuo kutoka kwa wafu siku ya mwisho, ndio tumaini la pekee la uzima na thawabu. NCHI ndio mahali ambapo wokovu mkuu wa Mungu utadhihirishwa. Huu ndio ujumbe wote wa maudhui ya kipekee ya maandiko. Daudi, Suleimani na Yesu wanaungana kutilia mkazo jambo hili.

"Maana watenda mabaya wataharibiwa, bali wamngojao BWANA ndio watakaoirithi NCHI … Wapole watairithi NCHI (Zaburi 37:9-11).

"Tazama, mwenye haki atalipwa DUNIANI (Mithali 11:31). "Heri walio wapole, maana wao watairithi NCHI (Mathayo 5:5)

Hakuna maelezo rahisi, wazi na chanya kama haya! Yafaa kuwa waangalifu, imani yetu kwenye msingi wa mafundisho na sio tu kuegemea yale ya jadi. Ahadi ya Mungu kwa Kristo ni kuwa (watu wakewatakapokuwa warithi sawasawa naye) –

"Nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako" (Zaburi 2:8)

Yesu naye anawaahidi wale wanaomtii –

"Na yeye ashindaye… nitampa mamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma" (Ufunuo 2:26-27).

Kwa hivyo wanaonekana kwa namna ya ishara wakimwambia (Ufunuo 5:10)

“Ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juuya NCHI”

Hali ya nchi itakavyokuwa imetukuka imeonyeshwa katika Ufunuo 11:15

“Ufalme wa DUNIA umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele”

Inakwenda sambamba na yale aliyerekodi Daniel kwa kuongozwa na Mungu –

“Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, CHINI ya mbingu zote, watapewa watu watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milel, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii” (Daniel 7:27)

Matokeo ya kweli kwake Kristo mara ya pili imejumuishwa kwa tangazo la malaika wakati wa kuzaliwa kwake:

“Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na DUNIANI iwe amani kwa watu wote aliowaridhia” (Luka 2:14)

Kwa hivyo Yesu akawafunza watu kuomba:

“Mapenzi yako yatimizwe, hapa DUNIANI kama huko mbinguni” (Mathayo 6:10)

Angewafunza kuomba kitu ambacho Mungu hakuwa radhi kutenda? La hasha! Ni jambo la hakika na ambalo limeamuliwa kabisa. Mungu aliapa (Hesabu 14:21)

“Lakini hakika yangu, kama muishivyo, tena kama DUNIA hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA”

Ni kitambo tangu aseme hayo! Lakini siku hiyo itafika kwani Mungu aliapa. Hatima ya waovu ni kuangamizwa katika ulimwengu wa Mungu; sio kuwatesa katika hifadhi ya moto wa milele, kama inavyofunzwa katika madhehebu makubwa ya Wakristo bandia.

Daudi alisema (Zaburi 37:20)

“Bali wasio haki WATAPOTEA, nao wamchukiao BWANA WATATOWEKA”

Naye Paulo anatangaza (Warumi 6:23) kuwa “Mshahara wa dhambi ni MAUTI.”

KIFO – Kutoweka kwa watu wote –

Ndio njia ya pekee ya Mungu ya matokeo ya maisha ya dhambi: maisha ambayo hayatolewi kwa Mungu – “Maana yeye apendaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu.”

Lakini twaona watu wema na hata waovu wanakufa. Jibu ni kuwa kifo kinachowapata watu wote sio hauamulliwi na mahakama yoyote: sio mauti ya milele ile ambayo itakuwepo kwa wanaowajibika wakati wa hukumu Siku ya Mwisho. Mauti ya sasa inafungia tu maisha haya ya

mwili wa kufa. Kwa wenye haki, ni kamakulala katika Kristo, wakisubiri siku ya ufufuo(1 Wathesalonike 4:14-16) –

“Hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye “Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni… nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa”

Angalia kwa makini: “Wanaowajibika” ni istilahi inayotumika kuelezea wale ambao wamefanya utafiti na kufikia ufahamu wa mpango na kusudi la Mungu, wakubali au wakatae kutii matakwaa ya Mungu kwa wao kubatizwa.

“Wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka (Daniel 12:2). Kuna “mauti ya pili” ya mwisho na ya maangamizi (Ufunuo 20:6,14; 21:8). WAsio haki wataletwa mbele ya Kristo kwa hukumu. Na hukumu yao itakuwa hivi, watapata kichapo wanachostahli (maigo mengi au kidogo: Luka 12:47 - 48), halafu baadaye, kwa ukali na mapigo ya Mungu, waangamizwe kwa mauti. Kama vile Mungu anavyoonyesha katika Malaki (4:1)

“Kwa maana, angalieni, ni siku ile inakuja kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itwateketeza asema BWANA wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi.”

“Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele”(2 Wathesalonike 1:9)

- Ina maana ya maangamizi ya kabisa yasiyokaza kitu.

“Kiswahili kikiisha pita asiye haki hayuko tena” (Mithali 10:25)

“Waovu watatengwa nan chi (Mithali 2:22)”

“Maana bado kitambo kidogo asiye haki HATAKUWEKO” (Zaburi 37:10)

“Wote wasio haki ATAWAANGAMIZA” (Zaburi 145:20)

“Hell” ni neno linalotumiwa sana katika tafsiri ya King James Version kama Sheol kwa Kiebrania na hades kwa Kiyunani. Neno “hell” inamaanisha “kufunika” au “kuficha.” Ilitumika wakati mtu alipokuwa akiweka paa kwenye nyumba au alipokuwa akifunika kitabu. Maana ya sasa ya wanadini na watu wa makanisa ni mahali ambapo waliokuja huadhibiwa. Hili ni fundisho sahihi la Biblia.

“Hades” na “Sheol” ni maneno ya kiyunani na Kiebrania mtowaliwa, kila mojawapo ikiwa na maana sawia na nyingine. Katika Biblia iliyoandikwa na wazee wale 70, ambayo nit oleo la Kiyunani la toleo la Kiebrania – Agano La Kale, neno “hades” ndilo limetumika kila mara badala ya “Sheol”. Neno hili latokezea katika Agano Jipya wanaponukuu kutoka katika Agano La Kale (Matendo 2:27, 1 Wakorintho 15:55). Kama “Sheol” watafsiri wametumia neno “hell” au kaburi/ kuzimu kwa raha yao wenyewe.

“SHEOL” (“mashimoni”) inatokea katika Agano La Kale la Kiebrania mara 65, na katika King James Version limetafsiriwa “grave” na “hell” mara 31 kila mojawapo, “shimo” – “pit” mara 3. Kutumia maneno haya mbalimbali kwatatanisha na inampendelea anayefanya kazi ya kutafsiri tu.

Wenye haki na wasiohaki wote wanalala pamoja (Yakobo, Ayubu, Shimei, Joab, “Waovu,” n.k. Mwanzo 37:35; Ayubu 3:17-19; 1 Fal. 2:6-9; ZAburi 31:17).

Ni mahali pa ukimya, giza, maangamizi, usahaulifu, katika mavumbi, hakuna kazi, hakuna hekima, hakuna mapenzi, hakuna chuki, hapana kumbukumbu (ZAburi 31:37; Ayubu 17:13 ; Mhu 9:10; Zaburi 6:5; Zaburi 88:11-12). Mchanganyiko wa mafundisho ya kipegani nay ale ya Kristo na mitume karne za mwanzo ndizo zimeleta matokeo haya kanisa la kisasa kufunza moto wa milele na adhabu na mateso kwa waovu.

Vifungu vingi vya maandiko –

Vilitafsiriwa kwa ufahamu wa maana halisi ya neno halisi ya neno asili alilotumia Mungu – inafhamika vema kabisa, na kuondolea mbali mafunzo maarufu, kama vile –

“Waaibishwe wasio haki, wanyamaze kuzimuni” (ZAburi 31:17)

Mimi Yakobo “Nitamshukia mwanangu, nikistikitika” (Mwanzo 37:35)

“I (Jacob) will go down to the grave (Sheol) mourning” (Genesis 37:35)

“Kama kondoo wamewekwa kwenda kuzimu (grave, sheol)” (ZAburi 49:14)

“Hakuna kazi wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu (grave, sheol)” (Mhubiri 9:10)

“Maana mautini hapana kumbukumbu lako; katika kuzimu (grave, sheol), ni nani atakayekushukuru?” (ZAburi 6:5)

“Kuzimu (grave, sheol) … gizani… uharibifu .. raha mavumbini (Ayubu 17 :13-16)

“GEHENNA” – “JEHANAMU” ni neno linguine katika AganoJipya, nenp la Kiyunani ambalo waliotafsiri wametumia neno “hell.”

Kwa msemo halisi, inamaanisha “Bonde La Hinomu” (Gai Hinnom), ikirejelea bonde lililokuwa nje ya mji wa Yerusalemu, ambapo moto wa kuchoma taka za mji na miili ya wahalifu iliyotupwa humo uliendelea kuwaka. Hakuna mtu aliyetupwa humo apate mateso akiwa hai, lakini maiti waliangamizwa kabisa humo. Kwa lugha ya mfano, inarejelea wakati ambapo hukumu ya Mungu iliyo kali itafika duniani hivi karibuni –

“Wakati wa kufumuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni… katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi… wao wasiotii…watakaoadhibiwa kwa MAANGAMIZI YA MILELE … atakapokuja (2 Thess 1:7-10).

“Mbingu za sasa na nchi (wanadamu walivyojipanga kwa sasa) … zimewekwa akiba kwa moto … zikilindwa hata siku ya hukumu nay a kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu” (2 Petro 3:7)

“Maana BWANA atakuja na moto … kwa moto na kwa upanga wake… Bwana atateta na wote wenye mwili; nao watakaouawa na BWANA watakuwa wengi” (Isaya 66:15-16).

Habari za Isaya za baadaye (Isaya 66) ni wakati ambapo Mungu “ataeneza amani na utukufu wake kwa watu wa Mataifa” hadi Yerusalemu; wakati; afanyize “mbingu mpya nan chi mpya”; wakati ambapo “wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu” (vifungu 12,22,23).

Tumepewa kionjo cha mambo yatakavyokuwa hatimaye, mambo makali wakati wa hukumu ya kusafisha ardhi hii katika Jehanamu ya kutisha iliyotokea Israeli mwaka wa 70 baada ya Kristo, wakati ambapo “mbingu na nchi” ya Israeli ilifagiliwa mbali kwa hasira ya Mungu. Ilifanyika wakati huo kwa sehemu ndogo lakini sasa itaenea ulimwengu mzima, na baada ya kusafishwa huko, pataimarisha amani ulimwenguni na haki kwa watu wote chini ya Yesu Kristo. Alisema:

“Aliye hai; name nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu (hell, hades, grave)” (Ufunuo 1:18).

Hii inaonyesha kuwa Kristo ndiye zawadi yetu, maana yeye ndiye – akirudi duniani – ana uwezo wa kufungua makaburi, na kuwarejeshea uhai hao waliokufa wakimtumainia. Kama malaika alivyomwambia Danieli (12: 2,13):

“Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele… Lakini enenda zako (Danieli) hata utakapokuwa mwisho ule; maana wewe utastarehe, nawe utasimama katika kura yako mwisho wa siku hizo.”

MUHTASARI

a) Ufufuo kutoka kwa wafu unawasubiri wote “wanaoajibika.”
b) Ufufuo Siku ya mwisho ndipo njia ya pekee ya kupata uzima baada ya kuingia kaburini.
c) Maisha ya milele baada ya ufufuo ndiyo zawadi kwa wale walio waaminifu.
d) Maangamizi ya milele yatawafika wote wasiokuwa watiifu – waasi.

MASWALI

1. Ni kwa njia gani zawadi yetu “imehifadhiwa mbinguni” wakati huu?
2. Zawadi hii iliyo “hifadhiwa” italetwa lini?

3. Mungu alimkadiria vipi Daudi, mfalme wa Israeli? Je, alienda mbinguni?
4. Hawa wanaotajwa na Paulo katika Waebrania ii ni watu wa nasaba ipi, aliposema hawajakamilishwa?
5. Wokovu mkuu wa Mungu utadhihirishwa wapi?
6. Hatima ya waovu ni ipi?
7. Mzizi au shina la neno la kiingereza “Hell” ni nini?
8. Nini maana ya neno hili la Kiebrania “Sheol”?
9. Nini maana ya neno hili la kiyunani “Hades”?
10. Nini maana ya neno la Kiyunani “Gehena” – “Jehanamu”?
11. Ni nani aliye na funguo za kufungua kaburi? Atafanya hivyo lini?
12. Nini maana ya istilahi hii “wanaowajibika” kama ilivyotumika katika somo hili?
13. Nini kitafanyika kwa wote “wanaowajibika” ambao wamekufa?
14. Watapata zawadi gani wale wote waliowaaminifu na watukufu kwa Mungu?
15. Nini mwisho wao wale ambao wameasi mapenzi ya Mungu?